- Kuonyeshwa picha au video za uchi au ngono;
- Kupigwa na kujeruliwa mwili;
- Kupewa adhabu kubwa/ngumu;
- Kutishiwa na silaha kama bunduki au kisu; na
- Kufanyishwa kazi kwenye biashara, mashambani, migodini, maduka, sehemu za kuuza pombe, migahawani, hotelini na majumbani (wafanyakazi wa ndani).

Toa taarifa juu ya vitendo vya ukatili ambavyo wewe au watoto wengine wanapitia

Sheria ya mtoto ya mwaka 2009 inamtaka mtu yeyote mwenye sababu ya kuamini kuwa mtoto amefanyiwa ukatili au unyonyaji, kutoa taarifa. Hakikisha haufumbii macho ukatili dhidi yako au watoto wengine kwa kutoa taarifa ili kuokoa maisha. Toa taarifa juu ya vitendo vya ukatili kwa:

- Mzazi au mlezi wako
- Mwalimu unayemuamini
- Jirani unayemuamini
- Viongozi wa serikali wa eneo husika
- Viongozi wa dini na wa kimila
- Timu za usalama wa mtoto
- Afisa wa ustawi wa jamii
- Polisi kata au dawati la jinsia na watoto
- Kituo kinachotoa huduma za afya
- Mashirika yanayotetea haki za mtoto
- Watoa msaada wa kisheria
- Piga simu bure namba 116.

Usikae kimya!

Toa taarifa na kuomba msaada endapo wewe au mtoto mwingine anapitia ukatili kwa ustawi wa watoto, jamii na taifa kwa ujumla.

Mawasiliano
Mradi wa 'Access to Justice for Women and Children / Society in Action for Equality' (SAFE)
Ofisi ya GIZ Tanzania,Nyumba Na. 65, Barabara ya Ali Hassan Mwinyi, Dar es Salaam, Tanzania
safeproject@giz.de

Je Unajua Haki Zako?

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA | WIZARA YA KATIBA NA SHERIA

german cooperation DEUTSCHE ZUSAMMENARBEIT

Implemented by giz Deutsche Gesellschaft für Internationale Zusammenarbeit (GIZ) GmbH

Haki za Mtoto

Mtoto ni mtu yeyote aliye chini ya miaka 18. Kama mtoto una haki sawa bila kujali jinsia, rangi, kabila, dini, hadhi au hali yako ya afya. Haupaswi kudhulumiwa na kutendewa vitendo vibaya na vya kikatili. Serikali, wazazi/walezi na jamii kwa ujumla wana wajibu wa kuhakikisha unapatiwa haki zako.

Haki za mtoto ni pamoja na:

1. Haki ya kuishi

"Nina haki ya kuishi kwenye mazingira mazuri, kulindwa na kuendelezwa. Serikali, wazazi, walezi, na jamii niwezesheni kupata lishe bora, huduma bora za matibabu, makazi salama, maji safi na salama, na mazingira bora."

2. Haki ya kuendelezwa

"Nina haki ya kupata elimu inayohusisha stadi za kazi, kucheza sehemu salama bila kuhofia ukatili na vipaji vyangu kuendelezwa. Mila na desturi zinazonizuia kupata haki zangu zinapaswa kutokomezwa."

3. Haki ya kulindwa

"Nina haki ya kulindwa dhidi ya kunyanyaswa na kubaguliwa, ukatili wa kimwili, kingono na kihisia, unyonywaji kupitia ajira za utotoni, pamoja na tamaduni na desturi kandamizi kama vile ukeketaji, ndoa na mimba za utotoni, mazingira hatarishi pamoja na kutelekezwa au kuachwa bila mlezi."

4. Haki ya kushirikishwa

"Nina haki ya kutoa maoni na yazingatiwe hasa katika maamuzi yanayo athiri maisha yangu. Ninapaswa kushirikishwa katika ngazi zote kuanzia kwenye familia, jamii na taifa kwenye masuala yanayonigusa."

5. Haki ya kutobaguliwa

"Nina haki ya kulindwa dhidi ya vitendo vyote vya ubaguzi unaotokana na jinsi, utaifa, rangi, dini, lugha, hali ya kipato kama vile utajiri au umaskini, hali ya ulemavu, afya, mila, desturi au asili yangu. Wazazi, walezi au jamii msininyime fursa yoyote ikiwepo kupata elimu kutokana na hali yangu."

Ukiukwaji wa Haki za Watoto

Watoto wengi wanafanyiwa vitendo vya ukatili na unyanyaswaji. Hii inasababisha kushindwa kufurahia utoto wao. Ukatili dhidi ya watoto una athari kubwa kwa maendeleo yao kihisia, kitabia, kimwili na kijamii kwa maisha yako yote.

Aina ya Ukatili Unaoweza Kufanyiwa

- Ukatili wa kingono; ikiwemo kubakwa, kulawitiwa, kushikwa mwili (sehemu za siri, matiti au makalio) kwa namna isiyofaa, kupigwa busu na au kuguswa sehemu usiyotaka;
- Kupigwa picha au video za uchi;
- Kusafirishwa kwenda sehemu (nchi) nyingine bila uhalali;
- Kufanyishwa biashara ya ngono;
- Kupewa pesa au zawadi ili kufanya ngono;
- Kuitwa majina mabaya, mfano; mbwa;